

# 21st Century Scholars

## Wazazi wa wanafunzi wa darasa la 7 na la 8:

### Watoto wenu wanaweza kupata udhamini wa kuhudhuria chuo kikuu

Programu ya Wasomi wa Karne ya 21 ya jimbo la Indiana itawalipia wanafunzi wa jimbo hili ada za kuhudhuria chuo kikuu kinachokubalika katika jimbo la Indiana kwa muda wa miaka minne baada ya kuhitimu shule ya sekondari, kutegemea mahitaji yao ya fedha. Kutoka darasa la saba mpaka darasa la kumi na mbili, wanafunzi wanaunganishwa na programu na zana zitakazoweza kuwasaidia kufanikiwa kwenda chuo kikuu na kupata kazi baadaye. Wakati wakihudhuria chuo kikuu wanafunzi watapata msaada ili kumaliza shahada zao na kuunganishwa na nafasi za kazi nzuri. Wanafunzi wa jimbo la Indiana wa madarasa ya saba na ya nane wanaweza kutuma maombi ya kuingia kwenye programu hii ya Wasomi wa Karne ya 21 ikiwa mapato ya wazazi wao yanakubalika. Tarehe ya mwisho ya kupokelewa maombi ni Juni 30 wakati mwanafunzi yuko kwenye darasa yatumwe.

### Kama msomi, unaahidi:

- ✓ Kukamilisha Scholar Success Program (Programu ya Mafanikio ya Msomi) katika shule ya sekondari na chuo kikuu, kuorodhesha shughuli za kila mwaka wa masomo kukusaidia kupata mafanikio katika chuo kikuu na kazi.
- ✓ Kuhitimu kutoka shule ya sekondari iliyoidhinishwa na jimbo la Indiana na kupata diploma kwenye kiwango cha Core 40 au zaidi na GPA kutoka 2.5 hadi 4.0.
- ✓ Hutatumia madawa kinyume cha sheria, hutafanya uhalifu, na hutakunywa pombe kabla ya kufikia umri wa kisheria.
- ✓ Kukamilisha Free Application for Federal Student Aid (FAFSA) (Ombi bila malipo la msaada wa wanafunzi kutoka serikali) kabla ya Aprili 15 wakati wa mwaka wa mwisho wa shule ya sekondari, na kila mwaka katika chuo kikuu mpaka utapohitimu.
- ✓ Kutuma maombi kwenye chuo kinachokubalika cha jimbo la Indiana ukiwa mwanafunzi wa mwaka wa mwisho wa shule ya sekondari, na kujisajili kuwa mwanafunzi wakati wote ndani ya mwaka mmoja wa kumaliza shule ya sekondari.
- ✓ Kudumisha viwango vya Satisfactory Academic Progress (SAP) (Maendeleo ya masomo yanayokubalika) vilivyoweka na chuo.
- ✓ Kukamilisha masaa 30 ya masomo kila mwaka wakati uko chuo kikuu ili uweze kuhitimu kwa wakati.

### Jiandikishe kwenye mtandao Scholars.IN.gov na utoe taarifa hizi:

#### Apply online at Scholars.IN.gov and provide:

- Nambari ya "Social Security" ya mwanafunzi, tarehe ya kuzaliwa, na anwani .
- Nambari ya "Social Security" ya mzazi au mlezi, au "Individual Tax Identification Number".
- Mapato kwa jumla ya mwaka 2021 kwa wote wanaokaa nyumbani. Ukituma maombi baada ya Desemba 31, 2022, weka mapato kwa jumla ya mwaka 2022.
- Anwani ya barua pepe unayotumia (Kama huna barua pepe, unaweza kuipata ya bure kutoka Yahoo.com, Gmail.com, Hotmail.com, na Live Live.com).

#### 21st Century Scholars Program Miongozo ya Mapato (2022-2023)

| Household Size                                       | Maximum Annual Income |
|--|-----------------------|
| 2  | \$32,227              |
| 3  | \$42,606              |
| 4  | \$51,338              |
| 5  | \$60,070              |
| 6  | \$68,802              |
| Kwa kila mtu wa ziada katika nyumba, ongeza \$8,732. |                       |

Scholars@che.IN.gov

21<sup>st</sup> Century  
**SCHOLARS**  
INDIANA